# CHUO CHA USIMAMIZI WA FEDHA

## JARIDA LA HABARI

TOLEO LA KWANZA
SEPT.2020




# MAONESHO YA 15 YA VYUO VIKUU TANZANIA YAFANA ....

- Ziara Simiyu
- Nane nane
- Baraza la Wafanyakazi
- Michezo
- Tanzia

# IFM YASHIRIKI MAONESHO YA 15 YA VYUO VIKUU TANZANIA

**Kwa mara nyingine Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) pamoja na vyuo vikuu na taasisi mbalimbali zipatazo 67 ziliweza kushiriki maonesho ya 15 ya vyuo vikuu yaliyoratibiwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kuanzia tarehe 31 Agosti 2020 mpaka tarehe 5 Septemba 2020 katika Viwanja vya Mnzazi mmoja. Maonesho hayo yalizinduliwa mnamo tarehe 2 Septemba 2020 na Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt Leonard Akwilapo. Katika hotuba yake, Katibu Mkuu alitoa wito kwa vyuo vikuu na taasisi kujielekeza zaidi katika kufanya tafiti zenye lengo za kujenga msingi wa uchumi wa viwanda.**

**Aidha aliviagiza vyuo kufanya tafiti hizo pia katika sekta za madini, utalii, uvuvi, kilimo na teknolojia. Pia aliongeza kwamba hadi sasa serikali imeshatoa sh. trillion 1.03 kwa ajili ya kugharamia elimu bure. Kutokana na hilo, ongezeko la wanafunzi wanaopata elimu limekua kutoka 8.3 millioni kwaka 2015 mpaka 10.9 millioni mwaka huu (2020).**

**Wakati akifunga maonesho ya vyuo vikuu mnamo tarehe 5 Septemba, Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Vyuo Vikuu Prof. Mayunga Nkunya alisema kwamba Tanzania ipo uchumi wa kati, na inahitaji wasomi zaidi kuweza kuendelea kwa nchi kufikia uchumi wa juu na unaotegemea viwanda vyenye wataalamu wa kutosha.**


**Kwa Mawasiliano:**

**Mkuu wa Chuo**
**Chuo cha Usimamizi wa Fedha**
**5 Shaban Robert Street**
**S.L.P.3918**
**11101Dar es Salaam,Tanzania**
**Simu: 255-22-21112931/3/4**
**Barua Pepe: rector@ifm.ac.tz**
**Tovuti: http: www.ifm.ac.tz**




**Pichani ni baadhi ya wanafunzi waliohitimu kidato cha sita walipotembelea banda la Chuo cha Usimamizi wa Fedha katika maonesho ya vyuo vikuu yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi mmoja.**

**"Bi. Veronica Mironge akimhudumia mmoja wa mwanafunzi wa kidato cha sita alipotembelea banda la Chuo katika viwanja vya Mnazi Mmoja."**



# ZIARA YA NAIBU WAZIRI WA FEDHA KAMPASI YA SIMIYU

**Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Dkt.Ashatu Kijaji aliweza kutembelea eneo la Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kampasi ya Simiyu iliyopo kijiji cha Sapiwi Wilaya ya Bariadi mkoa wa Simiyu. Kampasi hii iliyoanza kujengwa mwaka 2019 imefikia hatua za mwisho za kukamilika ambayo imehusisha ujenzi wa kumbi za mihadhara, maktaba na jengo la utawala, daharia na nyumba nne za wafanyakazi. Mheshimiwa Naibu Waziri alifurahishwa na ujenzi huo uliofanyika kwa gharama nafuu. Chuo kiliamua kuanza ujenzi wa kampasi hiyo baada ya kuridhishwa kuwa kusogeza huduma za vyuo vya elimu ya kati katika kanda hiyo kutatoa fursa ya kupata soko kubwa katika Mikoa ya Mara, Simiyu na Shinyanga**



**Picha ya pamoja ya Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Ashatu Kijaji (katikati) akiwa na uongozi wa Mkoa wa Simiyu na baadhi ya viongozi wa menejimenti ya chuo alipotembelea mradi wa chuo huko Simiyu.**



**Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Ashatu Kijaji (katikati) akiwa na uongozi wa mkoa wa Simiyu na Mkuu wa Chuo prof. Tadeo Satta ndani ya ukumbi mmoja wa mihadhara katika kampasi ya simiyu.**

# MAONESHO YA NANE NANE SIMIYU

**Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kwa mara nyingine kimeshiriki maonesho wa Nanenane.Hii ni mara ya pili kwa chuo kushiriki maonesho hayo huko mkoani Simiyu katika viwanja vya Nyakabindi. Kati ya shughuli zilizofanyika ikiwemo kukitangaza chuo na shughuli zake, pia shughuli za usajili wa wanafunzi walioomba kujiuga na chuo katika ngazi ya cheti zilifanyika.**

**Vilevile timu maalumu iliweza kutembelea baadhi ya shule zilizopo katika wilaya mbalimbali za mkoa wa Simiyu ikiwemo Busega, Meatu, Maswa . Pia timu ilienda na mikoa ya jirani ukiwemo mkoa wa Mara. Jumla ya shule zipatazo 53 zilifikiwa katika mikoa ya Mara na Simiyu na fomu zipatazo 600 zilisambazwa.**




**Baadhi ya wageni waliofika katika banda la Chuo kupata taarifa mbalimbali za chuo.**




**Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. Antony Mtaka (mwenye suti ya kaki) akipokea maelezo kutoka kwa Mkuu wa Chuo Prof. Tadeo Satta alipotembelea banda la chuo katika maonesho ya Nanenane.**

# UCHAGUZI WA BARAZA LA WAFANYAKAZI

Chuo cha usimamizi wa Fedha kilifanya uchaguzi wa Baraza jipya la wafanyakazi litakadumu kwa kipindi cha miaka mitatu. Uchaguzi huo ulifanyika mnamo tarehe 14 Agosti 2020 na ulisimamiwa na mwakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira , Vijana na watu wenye Ulemavu Mwakilishi kabla ya kuanza uchaguzi alisoma kanuni mbalimbali za kufuatwa kwenye uchaguzi. Moja ya kanuni hizo ni kwamba mkuu wa chuo ni mwenyekiti kutokana na hadhi yake. Pia wapo wawakilishi wanaoingia kwenye baraza kutokana na nafasi zao ikwi-

Waliochaguliwa kuwa wajumbe wa baraza la wafanyakazi la chuo ni wafuatao: Bw. Michael Mwasambili, Bw. Boniface Alfaska, Dkt. Bupe Mwakyusa, Dkt. Richard Kiagi, Bw. Matimbila Lyuba, Bw. Juma Kibacha, Bi. Theresia mendoza, Bw. Hamza Shaban,Dkt. Mastidia Byanyuma, Dkt. Edwin Kwesigabo, Dkt. Valeria Kyumana, Bw. Frank Kitende na Bi. Zubeda Chande.



Wajumbe wateule wa Baraza la Wafanyakazi la Chuo katika picha ya pamoja.

# MICHEZO




**Timu ya mpira ya IFM ikiwa kwenye picha ya pamoja kujiandaa ya mechi dhidi ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwl.Nyerere iliyofanyika katika viwanja vya Uhuru.**

# TANZIA



**Uongozi wa chuo cha Usimamizi wa Fedha umesikitishwa na kifo cha Mhadhiri wake Dkt. JOSEPH MABULA KIHANDA (pichani). Marehemu Dkt. Kihanda alifariki alfajiri ya jumanne tarehe 18 Agosti, 2020 katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Marehemu Dkt. Kihanda alizikwa nyumbani kwao wilayani Misungwi, mkoani Mwanza tarehe 22 Agosti 2020. Marehemu Dkt. Kihanda pamoja na kuwa mwajiriwa wa IFM pia aliwahi kuwa Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia 2014 hadi 2019.**

**Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema**

**Amina**